

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION_(CKRC
)**

VERBATIM REPORT OF

**CONSTITUTENCY PUBLIC HEARINGS
HAMISI CONSTITUENCY
NINEVEH MISION CHURCH_**

ON

MONDAY, 5TH AUGUST 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS
HAMISI CONSTITUENCY NINEVEH TOWN HALL**

Present

Com. Hon Phoebe Asiyu
Com. Ahmed Ida Salim
Com. Kavetsa Adagala

Secretarial in Attendance

Maimuna Mwidau - Programme Officer
Caroline Kihara - Assistant Programme Officer
Josephine Ndingu - Verbatim Reporters

Meeting was called to order at 10.30 a.m. with Com. Hon. Phoebe Asiyu in the Chair.

Com. Hon Phoebe Asiyu: You are very dull. Mchangamke at least tunataka tuanze this forum na tunaomba msamaha kidogo tumechelewa kidogo juu ya shughuli ingine ambayo tulikuwa nayo. Sasa kabla ya kuwanza mkutano nitamwita Reverend Henry aje atuombee. Karibu Reverend.

Asante sana kwa rehema za Baba wetu wa Mbinguni, tusimame tuombe. Asante Baba wetu wa Mbinguni katika jina la Yesu Hallelulah Jehovah asante, kwe mwenyekiti ya Commission na wote ambao wamefika, Hallelulah Jehovah bariki mkutano huu, uwongoze mbele na nyuma katika jina la Yesu. Uongoze mbele na nyuma katika jina la Yesu. Ongoza ma-pastor wetu ambao wako hapa, wazee, wanakamati, O'Jehovah ongosha hata Mhesimiwa, wote Bwana Councillors wetu, katika Teri Location waongoshe. Na utuongoze sisi wote katika rehema zako. Asante, asante kurudisha rehema hiyo, bariki mkutano na asante sana kwa kanisa hii, ubariki kanisa hili, na Bwana bariki jengo hili ukiwa wewe Yesu ndiyo msingi, wewe ndiye mjengaji, bariki wote na Waalimu wetu, Headmasters, na wote Education Officers, wale wamefika hapa, na tena Bwana tunakumbuka hospitali yetu iko mikoni mwako, asante kwa Commission iendelee katika rehema, katika jina la Yesu Kristo Mwokozi wetu. Amen. Asante sana, Asante sana.

District Coordinator: Asante sana Reverend kwa kutuombea, sasa tutaendelea na mkutano wetu. Na watu wa Hamisi vile manavyojua vile tumekuwa tukiwatembelea sana, kwa mambo ka Katiba tukiwafundisha tukiwambia ya kwamba Kenya iko saa hizi inarekebisha Katiba yake na mnatakikana mu-participate fully. Sasa watu wa kwanza sana kwa hii district mimi kukutana nayo wakiwa already active kwa mambo ya Katiba, walitoka kwa hii Constituency ya Hamisi, kwa mfano huyu Reverend tulikuwa naye tangu mwanzo kabisa vile tulikuwa Kaimosi, na Commissioner Mutakha Kangu. Sasa tutaendelea nani nataka kuwashukuru kwa kuwa na bidii sana kwa kuhudhuria mikutano yetu ya kufudisha na pia kuandika maoni na kujitokeza kwa wingi kuweza kutoa maoni kwa Commission, siku ya leo.

Ningependa pia kuwajulisha ya kwamba kwa hii Constituency, tutakuwa tuko hapa leo, kesho tutakuwa Kaimosi Friends College of Technology, na Wednesday tutakuwa Hamisi Catholic Church na hizi venue zote ni zenu nyinyi kutoa maoni yenu kwa Commission. Sasa bila kwenda kwa mengi nitapenda kuwajulisha wale ambao nimekiwa nikifanya nao kazi apart from Civic Education providers wale wako, ningependa kuwa introduce Kamati ile ambayo nimekwa nikifanya nayo hapa.

Wapi Reverend Mayathi just come. Sasa huyu ambaye tumesimama naye hapa, ni Reverend Tomas Mayathi na yeye ndiye mwenyekiti wa Kamati ya Hamisi Constituency Committee. Reverend Mayathi amekuwa anafanya kazi kwa bidii sana na Kamati yake, na kuhakikisha ya kwamba wananchi wamepata elimu na pia wamejitayarisha kupeana maoni yao. Reverend I will give you this opportunity to introduce yourself and to greet the congregation and also to introduce your committee. After which take the microphone.

Reverend Mayathi: Asante sana Madam Coordinator. Wahesimiwa ma-Commissioner wetu, ma-bibi na ma-bwana, wazee kwa wale ambao ni makamo na vijana wako na wanakuja, nawa salimu wote hamjambo. Hamjambo tena. Mimi nikisema ni shukrani, kuwapokea nyinyi hapa, ili tuungane katika kushiriki kuandikisha mpya Katiba yetu. Ma-Commissioners wetu wako hapa kwa ajili ya kupokea maoni yetu na wangelipenda tujisikie kwamba Katiba inatuhusu sisi, ni yetu na tungelifurahia kuona mwongozo wa nchi yetu nzuri kesho na kesho kutwa kwa sababu ya Katiba nzuri tunaandika. Kwa hivyo mumekaribishwa sana. Mjisikie mtakuwa na uhuru na wakati wa kuandika Katiba yetu.

Nataka kuwajulisha wanakamati tulio nao hapa tafadhali wanakamati walio hapa wasimame. Kule mwisho juu ni Madam Waithiria Mrs. Itheria ambaye ni mwenyeji wa sehemu hii na akiwa ndiye hasa alituweshesha kuweka mandalizi haya. Anayefuata ni Daktari Seroney, Seroney naye pia ni mwenyeji wa sehemu hii, zaidi akiwa anatoka Tamwaha na yeye ni mwana-kamati ametuwezesha sana katika mipango yetu ya Hamisi. Yule Bwana ni Bwana Madegesio, Madegesio ndiye amekuwa akituwezesha kuwasiliana kwa njia ya maandishi, yeye ndiye amekuwa mwandishi wa kamati yetu ya Hamisi Constituency Constitutional Committee. Na mama huyu amesimama ni mamama Elizabeth Olando naye pia hatoki mbali na hapa, yeye ni mwanakamati pia wa kamati yetu ya Hamisi. Kuna wachache ambao hawako hapa, mmoja nimepokea ripoti ana kesi kotini Bwana Hamisi hayuko hapa. Atakuwa nasi baadaye, halafu wengine kwa shughuli nje. Kwa hivyo nasema ni asante kwa nyinyi wote ma-Commissioners wetu karibuni sana nafikiri mumesha julishwa kwa, majina. Wenyewe watajijulisha. Asante sana. Basi karibuni sana.

Pole kwa mhesimiwa Khaniri ambaye kwa sababu ya shughuli ambayo imekubadhiri Nairobi, sasa tisa za leo, hukuweza kuwa nasi, lakini amekuwa hapa. Amekuwa hapa na kwa vile tulikuwa bado tuko katika hali ya kujitayarisha, basi ikambidi aondoke mapema ili apate kufika Nairobi mapema. Kwa hivyo amewacha document hapa, amewacha ripoti yake hapa, tutapeana kwa ma-Commissioners tukishaanza. Asantni sana.

Maimuna Mwidau: Habari zenu. Jina yangu ni Maimuna, mimi ni programme officer, kutoka CKRC pamoja na mimi niko

mtu wa ku-recordi maoni yenu ambaye anaitwa Josphine Ndungu. Na yule ambaye atakaandika maoni yenu anaitwa Caroline.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Kwa niaba ya Commission ambayo inatekeleza mambo ya Katiba mpya, ningependa kuwakaribisha sana sana katika mkutano huu wa leo hapa Hamisi, na kuwapa pole kwa kuchelewa kidogo kwa vile tulikuwa kwa ofisi ya DC asubuhi, ndiyo tupate nafasi ya kuingia hapa Hamisi. Ningependa kabla ya kundelea, kujulisha wale ambao tuko na wao hapa juu kwa upande wangu wa kulia ni msichana wenu mnamfahamu vizuri Kavetsa Adagala ambaye ni mwalimu katika Chuo Kikuu cha University ya Nairobi na ambaye pia ni Commissioner kwa Commission hii ya kubadilisha Katiba.

Com. Adagala: (Kiluiya).

Com. Hon Phoebe Asiyu: Upande wangu wa kushoto ni tena mwalimu, tena ambassador wa Kenya katika nchi ya Skandinavia naye ni Professor Salim ambaye ndiye anaongoza Panel hii yetu ya hapa.

Com. Salim : Hamjambo nyote.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Mimi ninatiwa Phoebe Asiyu. Zamani nilikuwa kwa Bunge na sasa niko kwa Commission hii na wenzangu hao wawili tumekuja hapa kusikiliza maoni ya watu wa Hamisi. Munajua mbunge ilifanya vizuri kupendekeza kwamba Commission isikae kwa ma-town kuzikiliza maoni ya watu wa Kenya na wakapendekeza ya kwamba tufike kwa Constituency ya Kenya na kushikiliza maoni ya watu. Kwa hivyo ni siku muhimu sana , siku ya leo, ambao tumekuja kusikiliza maoni yenu ambayo itaenda kutusaidia sana kuweka pamoja na maoni na fikira za watu wa-wengine wa Kenya, ili tufanye reporti ambayo ile ile ya hapa constituency itarudi hapa hapa, msome mtosheke, halafu tutawaletea pia report ya Kenya nzima ambao ikifika wakati hapo ikishawekwa pamoja mtachagua watu watano kutoka kwa kila district ambayo wataenda kukaa mahali fulani hapa Kenya, kujadilia mambo yale mtakuwa mmetueleza na kuzikilizana ili tutengeneze bill na recommendation ambayo itakuwa enacted na Bunge ili tupate Katiba mpya. Kwa hivyo safari bado ni ndefu lakini tunajuwa Mungu ikituangulia na nyinyi mkitoa mawazo mema yatasikizana na mawazo mengine ya watu wa-Kenya tutaweza kutengeneza Katiba mpya ambayo itafaidi watu wote wa Kenya, zaidi sana wale vizazi vijayo kwa maana Katiba ikiandikwa vizuri, mkitoa fikira zinazofaa itaweza kulinda nchi hii hata kwa miaka mia moja, mia mbili ijayo, vile Katiba za nchi nyingine zimefanya.

Tukianza kutoa maoni, tutapeana muda kulingana na vile mtu alivyo na maoni. Ninaona hapa kuna watu ambao wamebeba memorandum na wale ambao wanataka tu kuongea bila maandishi yeyote. Kwa wale ambao wana-memorandum hakuna haja kusema mambo mengi isipokuwa mta-highlight zile areas na zile mnaona ni very important, lakini mkumbuke kwamba hayo maandishi ambayo mumeandika itakuwa kama properties yetu kutoka saa hii, leo, ukisha tupatia. Na kila umeandika yataenda kwa computer halafu itatusaidia sana kulinganisha watu wengine na kufanya analysis. Kwa hivyo usiwe na wasi wasi kwamba maandishi yako yanaweza kuwa yatapotea bila kushikilizwa au kujadiliwa bila kuwekwa kwa computer. Kila ambacho

mtakuwa mumeandika mimi nimesema kitaingia kwa computer na kitatusaidia kutengeneza ripoti ambayo itarudi hapa. Kwa hivyo usiwe na wasi wasi na mazungumzo malefu kwa maana utapoteza wakati wako na huku umeandika.

Pili ili kila mtu ambaye amefika hapa leo apate nafasi, na ninavyoona hii nyumba itajaa na watu. Na mchana viko na masaa kumi na mbili halafu kutakuwa usiku. Sasa ingefaa mtu ukija hapa mbele sema pendekezo tu usitutolee, usitupatie hadithi vile wazungu walikuja, juu ya ile Katiba imekuwa, vile watu wana shinda sana na mambo ya shamba, tuwambie kama ni mambo ya mashamba vile unapendekeza.

Kama mambo ya Serikali mpya vile itaundwa utueleze vile vile. Kama ni mambo ya vijana, mambo ya mitaa, eleza hayo tu. Lakini upendekeze tu vile unataka iandikwe kwa Katiba, lakini hadithi mrefu itakupotezea wakati na tutaangalia saa sana. Ukipewa dakika tano, uje pale useme jina lako, kama unajisimamia mwenyewe au unasimamia kikundi fulani, pia useme, halafu toa pendekezo lako moja, kwa moja, hara, hara kabisa ili tupate maoni zafi na kila mtu apate nafasi ya kuongea mchana wa leo.

Tutaanza na Bwana Isaac Arab Seroney, ambaye ataongea kwa group ya TGY, tena TC elders. Yeye atatueleza hizi group mbili ni nani, nani na maana hakuwandika majina in full. Bwana Seroney, umekaribishwa five minutes. Halafu utatupatia memorandum yako, maana ulinieleza umeandika tayari, hata hapo umeleza kwamba ulikuwa umeandika. So you have five minutes Bwana Seroney to put your views cross and let them be recommendation for the new Constitution. Thank you.

Just a minute. Ningependa kuuliza wale ambayo wanajiadikisha pale nyuma kwamba tumeanza mazungumzo na kwa vile tuko ma machine hapa mbele hatuwezi kushika mambo yale ambao yataelezwa, kama mtakuwa kwa sauti hapo nyuma. Hata ingefaa mfanye registration kule nje kabisa, ili tuweze kusikiliza wale wanaongea hapa mbele kwa njia inayofaa. Unaweza kuendelea sasa Bwana Seroney.

Issack Arap Seroney: My names are Isaack Arap Seroney. I am representing a Soletai Youth Groups and at the same time there is a question I am representing by Perry Council of Elders. Thank you.

Preamble is necessary in found as good governance. Democracy, Resources, Culture, Love, Peace, Unity, Justice Unity and National Motto Harambee.

Rights of Minorities: Legality of minorities as personalities e.g. Terik people provides code numbers to use fully in registering of voters and issuance of Identity Cards and also use for National Planning.

Appointment and nomination in Land Commissions and both to safeguard individuals and communal land ownership.

Enforcement of international conventions and operational directives as recommended by World Bank for minorities should be recognized.

Provincial on alternative lands since they were ignored when others were being settled in settlement schemes like Indugare.

Entrench traditional authorities structures to ease burden and support administration.

System and Structure of Government: I am recommending Federal System of Government, with an executive President two Vice-Presidents one for internal affairs, one for external affairs, and I am also recommending a Prime Minister who is directly answerable to the President, who has got two Assistant Prime Ministers. All these is devolving power from the over-burdened Presidents. Also I am recommending the recommendation of two political parties of national outlook with substantial support, or substantial membership, with their own resources, in tribal Kenya.

Good governance under new Local Authority Structure, to establish autonomous local authorities, so that we revert to some of the by-laws of the Colonial Area which very useful.

Recognized independence of electoral and Constitution Review Process, such that registration of voters should be continuous, if there is any review act every five years.

Upholding of Constitutional Supremacy in Kenya, therefore clears supreme court to be guardian and to be interpreter of the Constitution.

Individual and Communal Rights, which have been disregarded: Promotional of social equity among vulnerable groups in Kenya, therefore guarantee Kenyans, disabled and otherwise equal opportunities in employment.

Guarantee of Social Economic Cultural of Rights of individuals and communities put measures to deal with questionable free enterprise and middle persons who exploit and even sabotage the economy of the country. These mechanisms are for ensuring productivity of its citizens in terms of efficiency and effectiveness. Thus improve.

Conservations of the Environment and Diversity: Our Environment is our heritage suitable and effective conservation methods be applied. Lands inter- boundaries and tree planting cause conflicts and in other cases, they interfere with water sheds which is our national resources.(inaudible) consider our views I believe this is a God send opportunity for the (inaudible) Thank you.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Thank you very much Mr. Seroney, I don't know whether any of the Commissions are any questions. But you were very clear and I am very grateful to you because you kept your time and you gave us very definite and substantive recommendations. Thank you very much. Now you can go over there and sign our register and also leave your

documents with our people at the back. Thank you very much. Can we now have Mr. Kipyegon Arab Mberia John.

John Kipyegon Arab Mberia: Majina yangu ni Kipyegon Arap Mbaria John. I am the Chairman (inaudible) Kenya in Kenya. And I am a nominated Councillor in Vihiga County Council and I have been a civic provider in this Constitution Review. Mr. Chairman, before I give you my memorandum, I want to give you highlights of what is contained in the memorandum.

I would like our Constitution to have the Preamble and the Preamble should reflect the governance of the people of Kenya like the National Motto of Harambee, peace, love and unity.

The former Constitution over sighted the rights of the minorities, marginalized groups, disabled in Kenya. But in particular today, I am talking about the Terik who are the minorities within this province. To begin with Terik that is why I wanted to elaborate thick and thin seem to be confusing, we (inaudible) Kalenjin speaking and we are the minorities and we like this Commission which is now prepared by the Kenyans that we be recognized and be called Terik and in order to be known properly we would like accorded a code number. Like any other minorities in Kenya like the Sengwe people, Dorobo, and others. Those are for purposes of registration of lands, censures, and so.

Com. Hon Phoebe Asiyo: You have three minutes remaining.

John Kipyegon Arab Mberia: Geographically, I have a memorandum with history which I will present to you and it will show you as shown in the map where the Terik moved from and where they came from up to where they are now.

When I come to the system of the government, I would like the Government which is coming to be a Federal Government. That is Majimbo. And the reasons not Unitary Government, the reasons is that we would like to decentralize the offices so that we can be given assistance or if there is any share, you understand..... (inaudible).

Com. Hon Phoebe Asiyo: Is there any one or two issues that you feel you have forgotten and you want to

John Kipyegon Arab Mberia: I would like to talk to something about Local Government. Local Government, I would like the Local Government to be ease that I would like to have (inaudible) the Chairman of the Country Council or Local Councils should be elected by the wananchi by the voters.

I would like Districts to have County Councils only and Municipal Councils to be within the province we should have some councillors from the County Council attending the Municipal Council rather than having mushrooms of county councils within the districts.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Thank you Mzee I see your time is up, but you have covered some very good grounds, we appreciate.

John Kipyegon Arab Mberia: I am presenting to you a memorandum which, has all the details, only few are given as highlights.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Thank very much Kipyegon Arab Mberia, can we have Japheth Amasinsa, you have a personal oral presentation. We give you five minutes.

Japheth Amasisa: Jina langu naitwa Japheth Amasiza. Maneno ya Katiba, habari ya mashamba inasemekana mwanaume na mwanamke wawe pamoja katika title deed. hiyo ni makosa.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Nani amesema hivyo.

Japheth Amasisa: Mimi na sikia au mi wewe.....

Com. Hon Phoebe Asiyo: Peana maoni yako. Kitu tunaka useme ni hii, “mimi sipendi wanawake na wanaume wawe na title deed” kama ni hiyo unataka kusema. Lakini usiseme umesikia inasemekana maana siyo sawa.

Japheth Amasisa: Haya. Sipendelewi mwanaume wawe kitu kimoja na mwanamke kwa title deed. Hiyo si vizuri, kwa sababu title deed inakuwa kwa jina la bwana na bibi wanakaa pamoja na bwana, wakipata watoto watakuwa pamoja kwa hiyo shamba.

Kwa bahati mbaya haijulikani bwana akitoweka akikufa bibi anarithi shamba. Bibi arithi shamba pamoja na watoto. Na bibi akitoweka, watoto wanambaki kwa shamba. kwa hivyo mimi naonelea shamba iwe tu kwa jina la mwanaume.

Manaeno ya vyama katika Kenya, viama viko Kenya vingi sana, naonelea vyama viwe vinne. Kwa sababu vyama arubani na zaidi ni vyama vingi sana.

Uchaguzi unatakiwa uwe na mwezi kufanya uchaguzi katika Kenya. Uwe kama mwezi wa December. Kutokea tarehe 27 au 28, iwe siku za kufanya uchaguzi, isiwe President anaweka siri katika roho yake ya kutangaza siku ya uchaguzi. Inatakiwa iwe mwezi fulani iyandikwe kwa Katiba ijulikane.

Wanawake inatakiwa sheria iwe kali ya kulinda ya wanawake, katika nchi yetu ya Kenya. Hasa watoto wasichana

wanafanyiwa maovu, hakuna sheria kali, inayochukiliwa kwa wanaofanya uhalibifu wa unajisi wa wanawake na watoto. Sheria iwekwe kali ya kulinda wanawake. Wanawake wakitembea watembea wakiwa uhuru katika nchi yao. Wasiwe wakutembea wakiwa na wasi wasi ya kufanyiwa maofu.

Uteuzi wa kuteuwa wenye viti wa ma-company. Kuwe na kamati au Commissioners au kamati fulani ya kuchagua watu kulinda ma-company, ma-parastatals. Isiwe Raisi ndiye anachagua hao watu wenye viti. Wachaguliwe na commission fulani.

Maneno mengine katika mahakama yetu ya Kenya, tuwe na sheria ya kulinda watu ambao hawana uwezo wa kifedha, ya kufanya ma-kesi katika mahakama. Kwa sababu watu ambao hawana pesa wakienda mahakamani watu wenye pesa wanachukua ma-Advocates wanaenda kusimamia kesi hata kama mtu iko na haki yake, na yeye hana uwezo wa kifedha ananyang'anywa mali kwa sababu hana Advocates. Napendelea Serikali itengeneze kamati ya kusimamia watu ambao hawajiwezi. Asante.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Umeifanya vizuri kutueleza mambo haya yote. Ulikuwa huna maandishi yote, kwa hivyo utaenda pale nyuma uweke sahihi yako kwa hiyo register yetu. Asante sana. sasa ningependa kumwita Bwana Henry Kipruto. Tafadhali fika hapa mbele mzee utoe mapendekezo yako. Halafu ninaona kama uko na memorandum ambayo utatuwachia. Asante sana. Kwanza aanza na jina lako halafu uanze mapendekezo.

Henry Kipruto: Asante sana mwenyekiti wa Commission. Mungu abariki mkutano mimi ni Reverend Henry Kipruto Kapkot. Mimi ni Pastor, na mimi ni member ya youth, ya Group inayoitwa Torik ka Teriki. Mimi ni member wa group hiyo. Mimi kwa mwenyekiti, katika Katiba mpya ya Kenya census, vitambulisho, viyandikwe Terik Kalejin. Si Tiriki Luhya.

Hilo ndiyo jambo kubwa la maoni yangu kwa group ya Torik ka Terik, Serikali ya Kenya iwe ya Majimbo.

Nchi ya Tiriki, Kalenjin, zilizotolewa nje, kutoka Tiriki Location na wa-Colony, zurundishwe kuwa pamoja na Terik Location. Maana hiyo ilikuwa ni uganja ya wa-Colony kugawanya Terik wasiwe na nguvu, wasiwe pamoja, wasiwe na lugha yao, wasiwe na culture, na Terik walipata shinda sana kugawanywa vipande vipande. Youth Terik Kalenjin wanaomba kwa rehema sana, Terik hiyo iunganishwe pamoja na iwe pamoja na Nandi. Nandi hawa ni ndugu zetu. Mipaka iko pamoja, lugha pamoja, makao pamoja, mito pamoja, mambo ya uchungaji ya ushirika pamoja, kwa hiyo wanaomba kwa rehema nyingi kwamba interpretation, yaani kugeuzwa kwa ubeberu wahumiza Kalenjin. Na Kalenjin wanaomba kwa imani na wandugu wote ambao tuko hapa ni Terik, tuwe pamoja na Nandi. Kuliko kugawanywa.

Mambo mengine ni kwamba Katiba yetu ya Kenya iwe na rehema ya haki kwa uchungaji ya wanyama ndege, wachungwe kwa mahali walipo, si vizuri kuhamisha wanyama katika mahali walipo. Si vizuri kuhamisha wanyama katika Kenya waende nchi

ingine au ndege. Kama vile Twiga na Punda Mlia kutoka Nandi, Soi Eldoret na ndege zetu kuhamishwa kutoka Naivasha ati ziende kufanya maisha pahali pengine. Naomba Committee na Kamati, waweze kufahamu mambo kama hayo, si vizuri kuhamisha hata ndofu katika Elgon kuhamisha kuenda kwingine, watengeneza mahali pao.

Jambo lingine naomba ma-kanisa yetu Katiba maana kama hii Ngene ya kusema ni ya damu hiyo si mambo ya kanisa, maana inapotesa watu wengi. Na mimi na youth group ya Terik, tulisikia wakitangaza Kipruto amevaa vizuri amepotea. Kwa nini watu wengi wanaanza kupotea katika Kenya, na Katiba ya Kenya iko wapi, kwa hivyo tunaomba Katiba mpya yako, mwenyekiti awe sawa sawa watoto wasiwe wakiotea. Alivaa nguo nyeusi, alikuwa na saa amepotea. Na tunasikiza na mtu amepotea. Watu gani wanaiba watu katika Kenya. Kwa hivyo tunaomba Katiba ya Kenya iwe imara na members wetu tena wawe imara. Watu wengi wameibwa, watoto wanaimbwa wana long wamepotea.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Ndiyo mzee tunashukuru sana sana, maoni yako. Tunajuwa utatupatia hiyo karatasi. Do you want to ask any question? Asante sana umefanya vizuri mzee Henry Kipruto. Sasa utuachie hiyo memorandum yako na halafu utuwandikie register yetu kwamba umeongea na sisi leo asubuhi. Kwa muda huu namuliza mama Judith kedogo ambaye ataongea kwa niaba ya Hamisi Women Group ulete memorandum yake hapa na kuongea na sisi. Kama yeye hajaingia mama Judith, Kedogo,

Henry Kipruto: Nimemaliza. Mumechukuwa kila kitu

Com. Hon Phoebe Asiyo: Umemaliza mzee. Ndiyo mzee tumechukuwa, tumeandika kila kitu. He has finished everything. Is that mama kedogo, okay have a sit there and make your presentation I see it is well written out, you will deposit with us so it becomes our property after you finish with it. Thank you very much. Do have a sit. Give us your name, those you are representing and then make your presentation in five minutes. Thank you.

Judith Kedogo: basi mimi niko hapa ku-represent

Com. Hon Phoebe Asiyo: Kwanza unanza na majina yako

Judith Kedogo: Naitwa Judithi Kedogo. Chairlady Gabduni Sub-Location, Gisambai Location, Tiriki West. Now niko hapa kusema jambo kuhusu wamama na watoto. Na ni reporti nzuri sana kwa sababu mimi ni mama na nina watoto. Kitu cha kwanza, vile mumesema na vile Katiba inaendelea, mimi kwangu naona inaendelea vizuri. Kwa sababu naona wama mbele yetu. Na siku zilizopita hatukuweza kuona mama mbele. Hapo nashukuru Serikali. Na rights za wamama hazijafikia kiwango sisi tunafikiria. Tunataka wamama wawe na rights karibu na ya baba, kwa sababu tulikuwa, hatutaki tuonekane mbele ya watu, lakini sasa tunaonekana kila mahali. Tulikuwa hata hatuoni, hatuwezi kuona DO. Hata chief, wamama hawakuweza kumfikia. Lakini saa hii hata ukienda kwa DC una right ya kuingia ndani. Wamama wanatakiwa wakiuliza kitu, hii Katiba iweke manani

sana, waone hawa mama wamepita.

Wawe na right ya kuingia kila mahali. Kwa sababu mwingine anasema, nikienda kwa DO ama hata nikaribisha. Hasa for example our DO is very kind and lenient he welcomes everybody, na nafikiri hii Katiba umemsikia sana, kwa sababu kila meeting tunakutana mpaka aje kusikia wamama wanasema nini.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Nina hofu sana mama Judith, mama Judith kwamba pengine dakika zako tano zitaisha kabla hujaongea mambo yako.

Judith Kedogo: Payroll share yake kama yule kwa sababu labda saa ingine vitu inakuja ama Serikali inafikiria kusaidia watoto na wana chaguwa. Wale ambao wanaweza kutusaidia na tunataka watoto wetu wote wawe vilema, wawe gani wasadiwe wapate kazi kwa sababu wana ubongo tu moja. Kwa hivyo nashukuru hii Katiba, iendelee kwa sababu inaonyesha dalili nzuri ya kusaidia.

Kenya yetu inaendelea mbele na tunaomba uchaguzi ujao, ukifanyika Muungu atuchaguliwe President an wengine ambao wataingia kwa mbunge. Na Muungu akituchagulia, na sisi tutafuata. Ni hayo tu Mungu awabariki.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asante sana mama Judith Kedogo embu weka sahihi yako pale na hiyo barua na hiyo karatasi pia weka hapo. Tumeshukuru kwa maoni hayo. Sasa ningependa Bwana Jamin Arap Kijo. Mzee Jamin kijo, wewe ni Arap Kijo, na wewe unataka kuongea juu ya ukataka Bwana Seroney akutafushiriwe. Sawa Sawa. Wewe kaa chini, na wewe pia ukae halafu Bwana Seroney akiongea na wewe unaongea kama yeye. Utaanza na jina lako mzee, ili iandikwe vizuri kwa recordi.

Jamin Arap Kijo: *Mwae ngfalek agobo sobenyin*

Transator: Anasema mambo yake kuhusu maisha yake.

Jamin Arap Kijo: *Kainenyun ko Jamin Arap Kijo.*

Transator: Naitwa Jamin Arap Kijo

Jamin Arap Kijo: *Mache komwa ngalek agobo ireyu.*

Transator: Anataka kusema mambo ya sehemu hii.

Jamin Arap Kijo: *Emoni keguren teriki .*

Transator: Anasema sehemu kusema kweli inaitwa Teriki.

Jamin Arap Kijo: *konngeten keny kogimenye boiyot nekeguren Bandamin*

Transator: Tangu zamani kuna mzee aliishi anaitwa Bandamin.

Jamin Arap Kijo:*kimi age ne kigiguren tomu.*

Transator: kulikuwa na mwingine alikuwa anaitwa Tom.

Jamin Arap Kijo:*komi age ne kigren ngamunya.*

Transator: Kulikwa na mwingine alikuwa anitwa Ngamunya

Jamin Arap Kijo:*Ngamunya kokisich korongorek.*

Transator: Ngamunya ndiyo alikuja akazaa rika inaitwa Korongolo.

Jamin Arap Kijo: *Kosich korongoro kikoime.*

Transator: Kongolo ikazaa rika inaitwa Kikoime

Jamin Arap Kijo: *kosich kikoime kipnyige.*

Transator: Kikoime ikazaa ingine inaitwa Kimiige.

Jamin Arap Kijo: *kosich age nekiguren nyongi.*

Transator: Ikazaa ingine inaitwa Nyongi.

Jamin Arap Kijo: *kosich ne kiguren maina.*

Transator: Ikazaa ingine inaitwa maina.

Jamin Arap Kijo: *Ngamunya komager nebo komager ane.*

Transator: Ngamunya rwakanza yeye hakuona, lakini aliona hawa baadaye.

Jamin Arap Kijo:*kiger korongoro.*

Transator: Aliona Ngorongoro

Jamin Arap Kijo: *Koger kikoime*

Transator: Akaona Kikoime

Jamin Arap Kijo: *kokimenye anyun teriki.*

Transator: Ndiyo alikuwa anakaa hapa inaitwa Teriki.

Jamin Arap Kijo: *kigemeny ireyu lakini kigiimech.*

Transator: Tumeishi hapa lakini tumeseka - tumesubuliwa

Jamin Arap Kijo: *makitinye kainet ne togu.*

Transator: Hatuna jina mbele ya watu

Jamin Arap Kijo: *Ago ireyu ko olinyon.*

Transator: Na hapa ni kwetu

Jamin Arap Kijo: *kigobwa muguga kobunu kibondo.*

Transator: Hasa mwingine alikuja anaitwa Muguga kutoka Kibondo

Jamin Arap Kijo: *kogurenke trikin.*

Transator: Akijiita

Com. Hon Phoebe Asiyo: Hebu kidogo, nina hofu kwamba ukitoa hadithi ndefu sana hautatapa nafasi ya kusema mapendekezo yako vile ungependa Katiba iandikwe. Sema mapendekezo juu ya Katiba mpya. Hiyo historia tumesikia, tumejuwa, lakini tunaka utwambia unataka twandike namna gani Katiba mpya.

Jamin Arap Kijo: *amache kenaanale a terikyot.*

Transator: Anataka ajulikane yeye inaitwa Terik ni wa kabila wa Terik.

Jamin Arap Kijo: *lagok che kigosomanso komasiche kasit.*

Transator: Watoto hata wale waliosoma kwanza hawakupata hata kazi.

Jamin Arap Kijo: *kuren Nandi ago magigochin.*

Transator: Wanaitwa wa-Nandi na sio hivyo huwa hapatiwi.

Jamin Arap Kijo: *okot kwo vihiga kosom kasit komakigochin kilejin kwenda huko.*

Transator: Hata akienda Vihiga aombe kazi hawezi akapewa anambiwa enda huko.

Jamin Arap Kijo: *ui Nandi.*

Transator: Nenda Nandi.

Jamin Arap Kijo: *Makimache okot kenai ke ki Tiriki.*

Transator: Hata anataka asijulikane sisi ni Tiriki kama wengine

Jamin Arap Kijo: *kimache kipandet netinye karnet mo nibokawaida.*

Transator: Anasema anataka kipande ya chuma, siyo hii ya kawaida.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Nafikiri nafaham mzee vile unasema.

Jamin Arap Kijo: *choton chehuk kityok.*

Transator: Sasa mambo yake ni hayo tu.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Tumeshukuru sana, hata kufika kwake, kwa kuongea na sisi na tumeandika yale aliyosema na pia machine imechukuwa. Asante sana mzee Jamin. Sasa ningependa kuwaelesha hivi, sasa zile mtu akiongea hapa mbele, kama manaongea hapo nyuma machine haiwezi kunasa sauti yake vizuri. Kwa hivyo ningependa tunyamaze kabisa mtu akiongea, ili tumpe nafasi, machine ishike sauti yake kwa njia inayofaa nasi pia tuweze kumsikiliza vizuri tukiandika maoni yake. Kwa wakati huu kuna huyu mama Tabitha Ruvai, ambaye ametoka kwa Umoja Women Group ambaye anataka kuongea na sisi. Tafadhali uje hapa mbele mama Tabitha utueleze juu ya Katiba mpya. Kama Tabitha hayuko, Mama Rispa Jamira, Maendeleo ya Wanawake Women, kutoka Vihiga. Rispa Jamira. Anza na jina lako, halafu ndipo uendelee kuongea.

Rispa Jamira: Mimi ni Rispa Jamira, natoka Tiriki West, Vihiga District, Maendeleo ya Wanawake. Vyama vya utetezi, viwe na uhuru visipigwe marufuku. Kwa sababu inatakikana kila chama kiwe na nafasi yake ya kutangaza kwa Radio au mahali wameenda. Na ma-sharti ya kuandikisha vyama yasiwe magumu. Vyama ambavyo havitakuwa na wambunge wanne wasikubaliwe kupiga kura wakati uchaguzi ujao. Baada ya kila miaka tano, lazima uchaguzi uwe kwa kila chama. Kwa sababu kuna vyama vingine ambavyo hawafanyi uchaguzi. Baada ya kila mwaka chama ambacho hakitakuwa na mashilahi ya kitaifa kisajiliwe. Kwa kila chama wapeane 35% viti vya wanawake. Wanawake wanganganiye hivyo viti.

Kila chama kiwe na uchaguzi wa viti 35%, wanawake. Wamama wapewe elimu ya masinani ili wajuwe vile wataenda kwa uchaguzi au utetezi, wasiwachwe nyuma. Na mbunge au diwani, ambaye atatoka kwa chama chake na ende kwa chama kiingine, apigiwe, kura au asiende mara tatu akitoka kwa chama hii akienda kwa hii, apigwe marufuku, awe tu raia.

Katiba ikubalie wale wanaotaka kusimama kipekee, kwa sababu kuna watu wengine hawana chama, lakini wanataka wakisimama wapatiwe nafasi.

Na upande wa Raisi, mamlaka ya Raisi, Raisi asiwe mbunge. Awe tu Raisi kwa sababu ana kazi nyingi. Na Raisi apewe mamlaka yote kwa sababu atakuwa na wenye watamsaidia kazi. Wale tena wapewe mamlaka. Wasiache mamlaka yote kwa Raisi. Asante.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asante sana, asante sana Mama Rispa Jamira. Tafadhali weka sahihi kwa register yetu. Kwa sasa nitamwita Salome Ngoke. Salome Ngoke, karibu kwa kiti upeane.... kwanza uanze kwa majina yako yote, halafu upeane maoni yako, kwa dakika tano asante.

Salome Ngoke: Mimi ni Salome Ngoke, na nina kuja hapa ku-represent Maendeleo ya Wanawake Shiriki West Division. Na nikiwa kama Life Member wa Maendeleo Organization. Sasa the electoral nataka kupendekeza vile tuliandika Electoral

System and Progress. The system should be changed to increase women participation in Parliament by doing the following:-

Ensuring that parties have 35% women in leadership, and any key leadership position of parties.

Pendekezo ni reserving 35% seats for women in Parliament.

Candidates who fail to seek nomination in one party should not be allowed to seek nomination in another party.

A member who defects from a party and crosses the floor should lose his seat in Parliament or in Council. Hata wale wa Council nyumbani.

The party should plan and replace him immediately.

Constitution should ensure every public elective office retains 35% seats for women.

Establish key regional

Com. Hon Phoebe Asiyu: You Salome I am getting worried about because you are reading instead of giving us a highlight. Because we will take that paper and will read and put in our computer. Just give us the highlights. Your time is running out.

Salome Engoke: Okay. Sasa other groups that should have a representation in Parliament includes young people and those that are interested, wale ambo wanataka kuja, kama ni wanawake, wale ambayo wanataka waje na waje kwa hiari ndiyo wapigiwe kura waendeleo.

Sasa nikiendelea mbele ni hiyo haki, the right of venerable groups: The Constitution, ya faa tukinagalia nilisema Electoral system, iangalie mashilahi ya wanawake. Wale ambao wataendelea kupiga kura, wale ambao hawajui kuandika waonyeshwe la kufanya wakati ambao wanapiga kura. Kwa sababu hatuwezi kupenda wale ambao wanaonyeshwa piga ndovu kama yeye alitaka kupigia ndizi. Na watoto nao wale ambao right yao, wale ambao wako njiani kama street children hao wakubwa wetu wajaribu, Serikali yangu kuwaleta waende kusoma. Watoto watoke kuzurura kuwa maduka kwa njia, wakiitwa street children.

Na wale ambao hawajiwezi, disabled, yafaa wasidiwe vilivyo, kama hawa ambao kwa sasa wana ugonjwa wa ukimwi, wasaidiwe na Serikali yetu, wawekwe mahali watibiwe. Na wale wamezeeka, wame-retire, tafadhali tena nao wasaidiwe, tena wawekwe mahali pao. Asante sana.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Asante sana Mama Salome Engoke, tafadhali peana hiyo documents yako pale na uweke sahihi

kwa hiyo register yetu na tumeshukuru kwa maoni yako. Julia Musasia, hebu kuja hapa mbele. Tumefurahi sana tumepata akina mama wengi. Kuingineko ilikuwa shinda sana kuwapata. Kaa pale chini wewe unasimamia Vibugi Self Help Group, halafu upeane jina lako kwanza mama, halafu uongee nasi.

Julia Musasia: Jambo, mimi Julia Musasia nasimamia kikundi cha Jigoji Umoja Self Help Group na pia Wakunga Baja Help Group. Hapa kuna memorandum ambayo walitoa naenda kusoma kuhusu views walizotea

Walipendesa ya kwamba nobody should be retrenched in Kenya instead, one to retire on her own will.

All Kenyans trained by Government of Kenya Institute, should be employed by the Government.

All HIV victims should be separated.

All street boys and girls to be cared by the Government example in educating them, in getting treatment.

If a woman gets maternity leave her husband should also take leave to care for her.

All TBS, Traditional Birth Attendants, mothers and CBD's –Community Based Distributors, to get enough materials from Government for their work and at least get small salary.

If a boy pregnate a girl they should all leave school.

HIV seminars (tape noisy and inaudible) kuhusu huu ugonjwa, kukiwa na Seminars na Cinemas all over the locations.

All crossed factories in Kenya operate so as to enable our children to get jobs examples KMC Kenya Meat Commission, ile ilifungwa, KCC na many others.

Electricity to be supplied in Rural Areas.

On Health facilities and storage of drugs – example tukiwa na hiyo stima tutakuwa na laboratories for blood test na tena tukiwa na hiyo electricity, tutakuwa na incubators for babies born before maturity time.

To encourage Jua Kali Sector, which is popularly dependable by Kenyans.

At least one ambulance in Health Centres for Emergencies.

Milk to be supplied in Primary School as before.

Canning should be abolished in all school, instead other punishment to be given.

Gender equality in Kenya example in Education employment and in leadership.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Naona umeandika kila kitu vizuri. Pengine useme moja tu ya muhimu.

Julia Musalia: Ya muhimu hapa mbili ni if a woman does TL yaani mwanamke akifunga uzazi yaani tubo-litigation a man should also do vasectomy. Hapo watasaidiana waishi maisha mazuri.

Ya mwisho – yaani ophans and widows to be helped.

Anybody found with a rape case, should be dealt with accordingly. For example he can be jailed for life.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Thank you very much. Now you will give us your paper, and you sign our register. Thank you very much.

Julia Musalia: I hope you will consider our views.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Everything in views given to us will be seriously considered. Sasa ningependa H.P. Amatha, sijui kama ni Mr. or you have not indicated whether you are Mr or not but you are H.P Amatha. What is your first name. Hosea Philip. Asante Hosea Philip karibu, uchukuwe microphone utupatie jina lako kwanza na kwa maana umeandika memorandum hapa, zungunza kwa dakika tano tu halafu utupatie memorandum yako.

Hosea Philiph: Mimi ni Hosea Philiph Amatha retired Agriculture Officer. Mimi nimefanya na Tom Mboya kufanya original planning in the Ministry of Economic Planning, kuleta Kenya kuwa stable. Mimi, Commissioner, nataka Constitution munayoandika iwe tayari by December. Tuko katika transition and it must go with the new Constitution. Na nataka the new President awe na 12 ministers. We have no money to pay. We trim the Cabinet, iwe economical according to the strategy of Kenya Economy. I would like this Commission to be trimmed wabaki ambao watakuweco in the new Constitution to serve on regional development. Because we cannot run a Regional Government, it is better to run Regional Economy, ambayo Professionals wataanza kupanga mipango ya sub-location, wawe na representatives wao, kuendelea halafu Commissioners tunakuwa, tunakuwa na repretantive ambaye anaenda kwa Commissions, kwa sababu tumepata MP hapewi nafasi ya

kutosha kwa umaskini, and the only way tunaweza kuleta pesa au kuleta stability, we want rural industrialization, watu wa Kakamega wakiwa na Rural yao wa-youth wao ambayo wamekosa kazi, wapate kazi. Watu ambao kuna Regional Development hiyo Regional projects ziwe represented and the share of economy ya country – sharing the cake of this country it must be shared equally and the only way tunataka iwe na Commission ambao imekuwa represented in all levels from the grassroots ili tuwe tunaweza ku-export, mimi nime-export privately kutoka hapa kuenda in other lands nikapata gold medals.

Now we want to be open to Export Markets. Kutoka haa Nyangori, kutoka hapa Jablock we should have viable projects that should be well designed, to be represented in any open market in the world to reduce this instability.

I also want the judiciary to free and all the powers of the Presidency be reduced. Thank you very much.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Thank you very much Bwana Amatha, kwa maoni hayo mazuri tafadhali tuwachie memorandum. Kwa sasa nitamuita Bwana John Likuba ambaye ana represent Mumias Community, nyuma yake tutakuja na John Bor, halafu Nelly Ndeaka. Asante.

John Likuba: Kwa majina naitwa John Likuba, representing Mumias Community. hapa nina memorandum ambayo imeandikwa lakini nita highlight jambo moja ama mawili kuhusu mambo ya Business in our area and in Kenya as a whole.

Sisi kama jamii ya wafanya biashara, tungependa kwanza kama tunataka tuwe na uchumi mzuri, tunakataka tuwe na uchumi mzuri, tunataka katika Katiba yetu mpya mambo ya biashara katika nchi ya Kenya yalindwe ki-sheria. Pasipo pahali pa bidhaa kutolewa nchi za nje ambazo ni za hali duni ni zinakuja kwa kumwagiwa na zinanyima wa-Kenya nafasi za kazi, nafasi za kufanya shughuli zingine za kiabiashara, ningependekeza kwamba business in Kenya should be protected and should be placed in the hands of the Kenyans especially those young entrepreneurs who should be protected so as to come up and do business in affair and good atmosphere.

Jambo lingine ni kwamba, tungependa katika Katiba mpya ipeane uwezo kwamba katika ushuru wa Serikali, pesa zitengwe vizuri katika sehemu zote za nchi hii, ku-develop mambo ya biashara. Na hizi pesa ziketengwa ziwewe kwa ki-Katiba kwamba kutakuwa na wafanya biashara wenyewe, ama vyama vya wanafanya biashara zenyewe zikisimamia hizo pesa na pengine Serikali kufanya tu mambo ya ku-supervise. Lakini sio hiyo iwekwe kwa mkono ya mtu mmoja, ama pesa ziwewe katika jambo ama mkono wa mtu mmoja kuyendesha kugawa na kutekeleza. Ziwe matekeleza ya mambo ya biashara na nini yawekwe kwa mikono ya wananchi ki-Katiba na kisa fanywa namna hivyo, tunaolea hiyo mambo itakuwa ni mzuri na hayo yote nafikiri tumeweka vizuri sana katika memorandum ambayo tumeandika na kama mume tuhakishia kwamba mtaisoma na yote yatafanywa, sioni ni kwa nini kuharibu wakati mwingi, ningependa nipeane tu namna hivyo, halafu mtafanya yale mnataka. Asante.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asante sana, asante sana, Bwana John Likuba hebu weka hiyo memorandum hapo kwa meza, na tafadhali uandike register yetu. Bwana John Boor yuko. John utafuatwo na Nelly Indeaka yule wa widows and orphans. Karibu na uko na memorandum vile umeandika hapa, useme tu machache sana, halafu utatuwachia document hiyo yako, asante Karibu sana.

John Boor: Kwa majina na naitwa John Cheboi Boor. Maoni yangu ni kwamba we need preamble na ianze and “we the people of Kenya, governed by peace, love and unity”.

We need Defence and National Security Ministry. The President be the Chairman of the Committee, which includes the Minister for Defence and Natural Security – Chief of General Staff, three major generals, airforce, navy, ground artilaries and the Attorney General a member of the committee. The permanent secretary in that ministry be the Secretary. The committee thus formed to declare war or state of emergency.

Political parties: Political parties with more than one million registered members be registered as a Political Party. This political party should fund themselves during the general elections using funds obtained from membership fee. Public funds should be left entirely for development of infrastructure, public institutions schools, universities, health facilities, water, electrcity, roads, increament for teachers and civil servants salaries to reduce corruption.

Cultural ethnics and regional diversity and communal rights, all minority tribes, be identified by being given code numbers, for census and other purposes. Not to be called others. Their numbers must be known in the new Constitution. Employment opportunities, 40% of employment opportunities awarded to each districts, should be reserved for the minority, marginalised and disabled in that particular districts.

Nominated MPs and Councillors: these should be maintained and entirely be left for the minority, marginalised, and disabled community for province. The Local Authority should do likewise with the Councillors. They should be approved by the Parliament, and Local Councils, at that level.

Moja ni juu ya ma-kanisa: Tuna ma-kanisa ambayo wazungu, foreigner, ama missionaries watuletea walipo zuru Africa ama Kenya yetu. Napendekesha ya kwamba ma-kanisa ya reduce, warudishe ma-kanisa yawe machache sababu yamekuwa mengi sana nchini Kenya, ambapo yameleta mizozo. Napendekeza yawe kama kumi, nchini, watu wawe wakiabudu katika ma-kanisa kumi tu. Dini ya Islaam ikiwako ndani.

Pendekezo lingine ni juu ya mitihani ya watoto wa shule kuanzia darasa la kwanza hadi la nane ambalo unaweza kuona kila mtihani ukija kwa muhula tuna-register. Tunapeana pesa za kuenda kufanya mtihani. Napendeleza jambo hili lifutuliwe mbali watoto wawe wakifanya mtihani wa bure yaani, kwa mihula hiyo mpaka ule wa darasa la nane.

Na malizia kwa uteuzi wa viti viwili Assistant Chief na Chief: Wawe wakiteuliwa na watu kwa sababu gani, sababu watu ndiyo wanajuwa utu wa mtoto wao ambaye wamemzaa, kwa hivyo wana right kusema huyu ametosha na huyu la. Namalizia, zilikuwa tatu.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asanti sana. Kwa sasa ningependa kiwauliza hawa wafike hapa mbele. Bwana Husdon Kesenwa, atafuatwa na Solomon Amandiva, halafu hapo mbele pia Bwana Tomas Musinga afike, na Joshua Nyangwenyi.

Hudson Kesenwa: Kwa majina naitwa Hudson Kesenwa na nayafuatayo. Kwanza ningependekesha ya kwamba mipaka iliopo baina ya Province na Province ikae vile ilivyo, wala isibadilishwe kamwe.

Jambo la pili, minimum qualification ya civic candidate iwe form four 3rd division and above.

Lingine ni kwamba kwa vile kuna watu ambao wanavuruga amani hapa na pale, sheria ambayo inawaadhibu wavurugaji wa imani kama hao, iwe enhanced from the current status to life imprisonment. Wale ambao wameweka – wanavurugha amani baina ya raia, yaani inciters.

Lingine ni kwamba Parliamentary term ipunguzwe kutoka miaka mitano hadi miaka minne. Na pia tuwe na time-table kamilifu kwamba wakati fulani Bunge litavunjwa wala isiwe siri ya Raisi kama mambo yalivyo sasa.

Lingine ni kwamba wakati Bunge limevunjwa, kutokana kwa muda huwo mpaka wakati tutakapochaguwa lingine, Mkuu wa Sheria awe Raisi mshikilizi. Atekeleze wadhifa wote ule ambao Raisi ambao angefanya.

La mwisho ni kwamba ma-officer wa Provincial Administration kutoka kwa naibu wa Chief hadi kwa PC, wachaguliwe na raia. Asante.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asante sana Bwana Hudson. Sasa ninamuita Bwana Noah Muganya, kama yuko. Nime mwita mara ya pili sasa. Bwana Joshua Nyangweso hiyo ni mara ya pili nimemwita. Bwana Richard Amisi, na Juma Mboya. Hawa wote hawako. Okay Somolon Ngona yuko. Kuja uanze kuongea. Solomon akimaliza tafadhali Michael Kiptoo awe tayari, na Elizabeth Onyenza, halafu utafuatwa na Eddy Ilagonza.

Solomon Chomok: Mimi kwa majina yangu ninaitwa Solomon Chomok Arap Ngona. Niko na maoni kama ifuatavyo:-

Ningependelea hii Katiba ambayo tunaweka wakati huu, ya kwamba tukirudi nyuma kidogo kwa elimu, ningependelea ya kwamba elimu irudi kama zamani, kuanzia moja hadi saba, halafu nne, halafu mbili, halafu university. Hiyo ningependelea kama Katiba ya sasa ingerudisha hivyo.

La pili ningependelea katika Kenya yetu ya sasa, ya kwamba katika Sub-Location, tuwe na Health Centres za kuhudumia wananchi.

Ningependelea ya kwamba katika jumhuri yetu ya Kenya, ambamo tuko kabila arubaini na mbili, na ningependelea kazi na kabila arubaini na mbili haya, tuwe kila mu-Kenya awe ya kabila ndogo, au kubwa, mtu ambaye lazima aongoze nchi hii na hata

kamwe anatoka kwa kabila ndogo, hata kama anatoka kwa kabira kubwa, na pendekeza ya kwamba, Raisi awe akihudumu kwa miaka mitano.

La mwisho ningependelea ya kwamba Katiba ulinde utamaduni, watu ambao ni wa hapa Hamisi hapa tuko na utamaduni mbali mbali wakati wa Christmas, au mwezi wa nane, ningependelea hiyo, tuangalie. Kila mtu na utamaduni wake wa tohara. Asante.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Asante sana Bwana Solomon. Mike Kiptoo yuko, Maritim, Elizabeth Onyenga, nilikuwa nimewaita tena. Elizabeth yuko. Abbey Iragoza, wewe ni nani mzee, okay. Aggrey Musiega, Jamin kirege. Wewe unaitwa je mzee. Endelea tafadhali. Kaa chini utueleze jina lako, halafu uendelee.

Jamin Kirege: Kwa majina mimi naitwa Jamin Kirege Kimosi. Na kwa maoni yangu ambaye ningelipenda kutoa, ni kwamba kila kiongozi yote katika Kenya hapa, akitaka apewe nafasi ya uwongozi, lazima tujue ya kwamba yeye ana pesa ngapi katika account yake. Kwa sababu hiyo kitu inakuja kusumbua raia.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Hiyo tunaijwa Mzee. Ungependekeza kiongozi tujue mali yako.

Jamin Kirege: Mambo ya pili ambaye ningelipenda kusema ni kwamba misitu ambayo iko Kenya hapa, iko kwa wa-Kenya kwa jumla. Na wakati Serikali inapostawisha mashamba kwa watu wengine, wanasahau watu wengine, wanapatia tu wale watu ambayo hiwo msitu uko sehemu yao.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Ungependa nini.

Jamin Kirege: Ningelipenda wale watu ambao hawana misitu kwa area yao na ni wa- Kenya kwa jumla, wawe transferred kwa hiyo misitu, wapewe wapatiwe mashamba vile wanapewa watu wengine.

Ya tatu President apewe mamlaka ya vipindi viwili peke yake. Ni hayo tu.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Asante sana Bwana Jamin. Sasa ningependa hawa wafuate: Nathan Kigaro, Susan Ndiazi, mbona hawaji mbele, Ebewa Benjamin, Stell Mbuga, Agneta Igemile, Isaia Alenga, Elijah Bagaya, Florence Agano, Nabiri Karani. Nani wale nimetaja jina tafadhali. Mje hapa mbele halafu muongee. Wewe umekuja mbele sema jina lako na ukae. Unaitwa je? Benjamin Ebeiyo, kaa hapo uongee, utafuatwa na Elizabeth Misigo, halafu Stella Mbuga.

Benjamin Ebeiyo: Jina langu Benjamin Ebeiyo. Mimi napendelea wakati ambao sisi tulipata uhuru, tulibakia nyuma.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Sema vile unatake tuandike Katiba. Uhuru tulikuisha pata.

Benjamin Ebeiyo: Cha pili tuko na mawe hapa katika nchi hii na hatuna kazi. Tuna elimu lakini watoto wetu wanasoma. Lakini hakuna kazi, tutaweza saidia namna gani wale ambao wanasoma. Na kama kazi hakuna.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Ungependekeza nini kuhusu madini?

Benjamin Ebeiyo: Tupate wale ambao wanaweza kutusaidia, ili kutokana na yale mawe tupate kazi.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Endelea.

Benjamin Ebeiyo: Maana yake sisi tuko na mashamba kidogo, lakini mawe yako mengi.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Endelea, tumeandika hiyo, sasa fanya ingine mpya. Tumeandika mambo ya madini na ya mawe. Pendekeza ingine mpya.

Benjamin Ebeiyo: Ninapendekeza sisi kwa upande wa Raisi, tupate upande huu. Na hayo tu.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Asante sana. Katiba tukiandika tupate Raisi kutoka upande hii. Wa-Kenya hawakubali lakini tumesikia majadilio yako. Mama wewe ni Elizabeth Misigo. Kuja mbele Elizabeth. Elizabeth Misigo hakuna, wapi Stella Mbuga, Stella hakuna, wewe ni nani, haya kaa chini ongea.

Com. Adagala: (*in Luyia dialect*) Numuyanza vaandu va mumoloma, tafadhali watu wanazungumza. Watu ambao wanzungumza, tulieni. Endelea Stella. Stella Mbuga.

Stella Mbuga: *Inze kulita ni Stella Mbuga*

Translator: My names are Stella Mbuga.

Stella Mbuga: *Avavisandu, batali na nyia na ise dave*

Translator: The orphans.

Stella Mbuga: *Sivaveye no bukonyi da*

Translator: They have no help.

Stella Mbuga: *Vakunza butswa*

Translator : They are just staying.

Stella Mbuga : *Kukugenya mbo lwa serikali aveyo yenyeka ikukonye avana vene yava ivungelitsi ikukonye kuvungitsa vasome, ha noho bakonywe.*

Translator: The Government should help us, so that the children can be educated.

Stella Mbuga: *Na kenago kanyakitsanga lwandola avana nivagendagenda.*

Translator: That is the only problem that is disturbing me, when I see children just moving around idle.

Stella Mbuga: *Simbeye na mingi dave. Ni yako vutswe ndio*

Translator: I don't have much that is all.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Asante sana mama Stella. Agnetta yuko. na Isiah Alenga. Tafadhali kuja uongee. Bwana Isiah atafuatwa na Elijah Bagaya ambaye atafuatwa na Florence Anganu, na Ambili Karani kwa njia hiyo.

Isaiah Alenga: Kwa majina kamili ni Isaiah Alenga Bagaya. Ningependa upande wa elimu, turudishiwe elimu ya zamani, darasa ya kwanza mpaka saba na watoto wapewe vitabu bure.

Matibabu ningependa watu ambao wamepata ajali barabarani na kuumizwa na mikora wapate matibabu ya bure kwa hospitali zote, iwe ya Serikali ama ya kibinafsi.

Law Courts: Ma-Judge wapewe muda wa kukaa na case, isizidi mwaka moja.

Mashamba: Serikali ilipie mashamba ambayo yako karibu na barabara na yameharibiwa wakati inarimwa na makarabati kiholela.

Kenya Currency: Ningependa sarafu iwe ya Raisi ambaye alitanguliwa.

Vyama: Ningependa vibaki vitano baada ya uchaguzi. Ni hayo tu asanteni.

Com. Hon Phoebe Asiyu: Asanti sana Bwana Isaiah. Wewe unitwa je mzee? Elijah Mbagaya. Asante.

Elijah Mbagaya: Asante. Mimi kwa majina naitwa Elijah Ishia Mbagaya. Napendekesho langu la kwanza ni kuhusu elimu. Tunataka tuwe na elimu ya bure katika jamhuri yetu ya Kenya zamani .

Kwa upande wa matibabu, iwe tena bure. Kwa sababu kuna wengine wanapata ajali barabarani akipelekwa hospitalini anaulizwa pesa.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Tupatie maoni mengine.

Elijah Mbagaya: Na tena kuna wengine ambao wamepatwa na ajali ya moto tena wakienda hospitali wanalilizwa pesa na kumbe hukuwa na pesa wakati ajali hiyo imefanyika.

Na tunataka madaktari wapelekwe kwa kila hospitali za wilaya, na pendekezo lingine ni kuhusu machief, wawe wakichaguliwa kwa njia ya mlolongo.

Na pendekezo lingine ni wazee wa mitaa: Wazee wa mitaa wapewe mshahara, na tena pendekezo lingine kuhusu madiwani kuhusu madiwani, wawe wakilipwa mshahara mkubwa kwa sababu hao ndiyo wanakaribia wananchi kwa njia rahisi.

Pendekezo lingine ni kuhusu kazi. Mtu mmoja kazi moja. One man one job. Pendekezo lingine in kuhusu mashamba. Hati ya kumiliki mashamba ni ghali mno. Asanteni.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asante sana Bwana Elijah. Sasa namuita Florence Agano. Florence Agano yuko? Kama hayuko Habiri Karani yuko? Ameenda. Haya sasa Dishon Kigagwa. Wewe utafuatwa na Daniel Viozi. Halafu Ex-Councillor William Sambua kwa hiyo laini.

Dishon Kitagwa: Maoni yangu. My names are Dishon Kitagwa, as it has been announced. First thing I must have to comment on the Presidential inheritance. That should be omitted.

MPs issue: We are supposed also to get an MP from our people and we are supposed to elect ourselves.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Just give us your recommendations that will go along with. Just give us your recommendation, your opinion.

Dishon Kitangwa: Second I feel in schools from Standard one to eight should not to pay school fees.

On Business people should not be paying tax.

Com. Hon Phoebe Asiyo: You dont want people to pay tax, so where will the County Council get money to carry out services. What sort of business are you talking about. This business, all business.....

Dishon Kitangwa: Mostly on the small scales. Because that will uplift the poor people like us who are in the local areas.

Also on drinks, But busaa should be legalized.

On communications: Roads should be good to enable us transport our goods.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Okay Bwana Dishon, if you had just gone still made recommendation after recommendation you would have covered alot of grounds. But that is alright. What you have told us is also very useful. Please sign our book. Please do not go without signing our books. Daniel Liyosi, William Sambwa, please join us.

William Sambwa: My names are William Sambwa. Napendekesha ya kwamba katika Kenya hatutaki majimbo hata kidogo. Sitakubali hiyo majimbo hata kidogo.

Pendekezo langu la pili, sitaki mipaka ingine ya watu kudai Kitambua na Chepkoyai irundi Rift Valley. Hiyo mimi sitaki hata kidogo, ni jambao moja linaturudisha nyuma.

Pendekezo lingine, wakati wa Howard alifanya mpaka Rift Valley na Western. Kwa nini tena mipaka mingine ya pili itengenezwe. Hiyo ni mbaya.

Pendekezo la tatu: Divisional izitumie majina ya ukabila, kwa mfano kama Tiriki West na Tiriki East na yet tuko na Hamisi Division. Kwa nini hatuwezi kuwa na Hamisi West na Hamisi East.

Pendekezo la nne: Kama mtu anaoa ama msichana anaolewa, baba yake apewe kitu kidogo. Kuliko kusoma washikilizane tu halafu waowane. Lazima msichana aolewe.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Wacha kulazimiza wasichana waolewe. Kuna wengi siku hizi wanafanya kazi. Hawaolewi.

William Sambwa: Hii ni mila yetu waowe. Hata kama anafanya aolewe, kitu kidogo kwa wazazi.

Juu ya utawala, napendekeza, Chief, Assistant Chief, wafanyiwe mlolongo, kuliko kuletewa tu mtu.

Kazi ya Councillors, mtu ateuliwe ambaye ana ujuzi wa kazi hiyo, kuliko kusema mtoto. Hiyo si vizuri.

Nikimaliza, nadai Kamshenyere, Kapkeleki zirudi Western. Asante.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Wewe ulisema hutaki mipaka ibadilishwe kamwe. Sasa unataka ingine ibadilishwe sasa wewe una simama- msimamo wako ni mgumu. Haya basi asante sana.

Com. Kavetsa Adagala: Mzee kuna jina Tiriki constituency, kuna jina Hamisi constituency. Mumesikizana lipi linfaa litumike. Kwa sababu watu wengine wanasema Hamisi ni jina la mwarabu ambaye alikuwa anapitia huko, na we unasema Tiriki ni jina ya kikabila.

William Sambwa: Ya, sababu nikisema hivyo, Hamisi ni jina ambalo mimi nilizaliwa ikiitwa Hamisi. Hakukuwa na tatizo yoyote. Lakini wakati ya Tiriki East and Tiriki East ndiyo inaleta mzozo hapa. Kwa hivyo tunataka iwe Hamisi peke yake.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Haya mzee tumesikia maoni yako, tafadhali weka sahihi kwa kitabu chetu. Sasa ningependa kumwalika wana Fanuel Manela yuko? Na Jairus Adam Muriega, Jairus yuko? wewe uko na memorandum hutaongea utasema tu machache halafu utupatiye hiyo karatasi, maana umeandika.

Jairus Adam Liaga: Kwa majina Jairus Adam Liaga. Mimi ningependa kupendekeza yafuatayo:

Ufisadi: Hili ni jambo ambalo limerudisha maendeleo ya Kenya nyuma sana. Kwa hivyo ningependekeza sheria itolewe kali kuhusu wale wanaouhusika kuliko vile ilivyo sasa.

Pia napendekeza hii Commission ikimaliza kazi, tuweze kuwa na kamati ambayo italinda hii sheria ambayo munatunga.

Haki: Napendekeza haki iweze kufunzwa katika kuanzia primary hadi university. Kwa maana wengi hatujui haki zetu. Hiyo ndiyo njia moja, itatusaidia.

Pia ningependa kupendekeza koti mara nyingi huingiliwa na Serikali. Ningependekeza koti iwe independent ama ipewe mamlaka ya kujiamulia mambo yake peke yake.

Sheria kuhusu idara ya polisi: Ningependekeza ifanyiwe overhaul ama marekebisho kwa maana huko ndilo ufisadi umezidi zaidi. Kwa hivyo, basi asanteni. .

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asante sana mzee. Sasa ningependa kumwita Mary Luvavi, akifuatwa na Flora Omoke?, halafu atafuatwa na Reverend Simon Muhindi. Wapi Flora Omoke. Wewe ni Mary. Flora Omoke yuko?. Karibu Mary uanze, utueleze majina yako yote, halafu uongee.

Mary Luvavi: Asanteni. Mimi kwa majina naitwa Mary Kavetsa Luvavi. Ni mkaazi (inaudible) Sub-Location,

Tiriki West.

Ningependa ya kwamba wamama wapewe nafasi ya uongozi ikiwa kuna kazi wama pia wachukuliwe.

Ningependa hospitali Zetu ziwe za bure ili watu wapate matibabu.

Ningelipenda Title Deed za shamba pia wamama tuwandikwe ndani ya hiyo title deed. Twandikiwe Mr. & Mrs. kwa sababu huwa tunafinywa.

Ningependa elimu ya watoto wetu kuanzia darasa la kwanza mpaka la nane na kwenda secondary tusaidiwe watoto wasome bure. Lakini Secondary walipe kitu kidogo.

La mwisho ningependa hii tume ikimaliza kazi yake, wachague watu wawili mama mmoja na mwanaume moja waingie Bunge, ili wajuwe haya tunaongea yanatimizwa ama namna gani. Ni hayo tu Asante.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asante sana Mary kwa maoni hayo. Sasa nenda pale uweke sahihi. Reverend Samuel Muhindi tafadhali unaweza kuja sasa. And because you have a memorandum which you are going to read, you don't have to talk for too long.

Rev. Simon Muhindi: Thank you. Naitwa Rev. Simon Muhindi. Ningependekeza jambo la kwanza Electoral Commission ipate kupeana nafasi kwa Katiba mpya ili ya kwamba ipate kufuatilia mambo ya uchaguzi, kwa sababu katika uchaguzi, kuna hongo nyingi na watu hunua kura. Kwa hivyo Electoral Commission ipewe uwezo na Katiba hii kustaki mtu ambaye atakayehusika katika mambo kama hayo.

Jambo la pili: Ningependa ya kwamba Katiba hii ipate kutoa jukumu katika judiciary, maana tunaona ya kwamba kuanzia kwa Attorney General na Chief Justice, na Judges, hata Magistrates na Lawyers katika nchi ya Kenya, maana hayo ndiyo backbone ya nchi hii. Lakini vile inavyo haribika, the system, basi inakuwa ya kwamba nchi inaharibika. Ningependa Katiba hii itoe provision ikiwa wananchi wanaweza hata kugoma kwa ajili ya mambo hayo kwa sababu Attorney General ame-fail na system yake yote. Kwa hivyo Katiba itoe provision ya kwamba wananchi wanaweza kukataa na kulete mambo ya kuonyesha ya kwamba hali imeharibika.

Halafu jambo lingine kuhusu mambo ya Court. Law Courts katika Kenya ningependa ya kwamba katika kila division, kuwoko na magistrates, ili ya kwamba kesi zisiende mbali sana na watu, zifanyiwe katika division zao, na High Court iwe katika district, in each district kuwoko na High Court.

Halafu jambo la nne ningependa ili ya kwamba kuhusu mambo ya marriage, katika nchi ya Kenya hakuna haja ya DC kufanya registration. Bali tungependa ya kwamba watu – mtu ambaye anataka kuoa ikiwa ni mwanaume arudi nyumbani kwao. Aende kufanya registration yake katika ofisi ya Chief apewe marriage certificate. Na hiyo marriage certificate tungependa , ikiwa ana wanawake wake wote watiwe katika hiyo certificate ili anapofariki kusije kukawa na shinda. Na pasije pakawa na divorce katika nchi ya Kenya wala Katiba hii, kupeana provision ya divorce.

Halafu ningependelea clergymen katika Kenya wapewe pesa na Serikali kwa sababu wanafanya kwa wananchi wa Kenya. Thank you.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asante sana Reverend unasema ya kwamba wanawake wote wakiolewa na bwana mmoja wapewe registration, halafu unasema kusiwe na divorce. Na je kama mama kati ya wale wengi unasema wapewe registration hakai viziri na huyu bwana unataka akaye tu hapo.

Rev. Simon Muhindi: Dear Commission, najuwa ya kwamba kufuatana na mambo ya ndoa hiyo ni mapenzi ya mume na mke. Kwa hivyo wamependana. Ikiwa ni kuwachana sioni haja ya huyu mmoja kwenda kotini ili ya kwamba Serikali inampa licence ya kuwa ya kwamba ame divorce kwa sababu pale ambapo alipokuwa wawili koti haikuwako. Kwa hivyo naonelea ya kwamba iwe silence maana mambo haya yamefanyika mara kwa mara. Wanapeana divorce, later on baada ya miaka wanarudiana tena.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asante sana Mzee tumeshukuru. Kwa sasa ningependa kumweleza Elizabeth Olando, hii kitu unataka kufanya ufanye mwisho na tuko karibu kumaliza. Kwa hivyo tafadhali ugojee kidogo tu. Bwana Patrick Avrud yuko, Patrick Avrud, na kama yuko bona huongeei, unataka kuongea. Basi kuja, halafu utafuatwa na Amdavi Chanzu, na Kiverenge Hezoron, halafu William Madima. Wote waje wakae hapa mbele.

Patrick Avrud: Mimi kwa maoni yangu ningependa kutoa hii hoja ya kwamba ma-officer wote – wale wote wa Serikali ambao wasawahi kuhusika na mambo ya ufisadi ya faa – kwa majina ni Patrick Avrud kutoka Ivona Sub-Location.

I would like to propose that those civil servants who have ever engaged in corruption mishandling of the Government funds must be sued.

I would like our division to be divided into two equal parts. Because like now we justify that we have got Tiriki East and Tiriki West. Meaning it is a very huge division which should be divided into two equal parts in order to drive out the tribalism which in between the tribes.

I would like to propose that the Government , the devolution of power to the President must be emphasised. Powers of the

President must be divided that any person holding any credible responsibility in the Government should just hold just one duty but not more than that.

We must have gender equality in our states. We should not have discrimination.

We would like the Electoral Commission of Kenya, to increase the period of registration for voters' cards and also for the ID cards because the majority of youths especially from our Division have no ID cards and the voters cards. So I would like registration for IDs and voters to be a continuous exercise.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Thank you very much Patrick for those views. Is Amudavi Charles there?, and Kiberenge Hezron? Kuja kaa uongee. William Malima yuko?

Hezron Kiverenge: Kwa majina mimi naitwa Kiverenge Hezron, kutoka Ivona Sub-Location. Mimi nitaongea kuhusu wa-mbunge, ma-Councillors na ma-Ministers. Pendekezo langu ni kusema ya kwamba, hawa watu wote wasipotekeleza maendeleo kwa nchi zao, inatakikana mishahara yao isimamishwe, ili isaidie wale watu wenye wanawasimimia.

Kitu cha pili kuhusu ma-retired officers. Hawa watu tuseme wakipata retire yao, inatakina waende wafanye miradi, ili wasaidiye maskini na mayatima na watu fulani fulani na kadhalika. Na watu kama hawa unaweza kuwakuta tuseme Serikali imetoa contract fulani fulani, unaweza kukuta watu kama hawa wameshika hiyo kazi, na waki- shika hizo kazi sasa, wale vijana wamesoma kwa hiyo – sasa mimi napendekeza ya kwamba watu kama hao waadhibiwe inavyotakikana.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Hawa Asante sana Kiverenge umeongea tumesikiza. Timothy Mahagwa? Kuja uongea. Bwana Morogo aliongea Chief na akaenda. Kuna Morogo mwingine?

Timothy Mahagwa: Kwa majina naitwa Timothy Mahagwa Mahangiru kutoka katika Ikindu Village, Mwembe Sub-Location, Tambua Location.

My first objection is in the part of Presidency. The President should not have superpowers. The powers of the President must be reduced.

Retirement: In Permanent and Industry jobs when a man or employee has reached the retirement, it should not be supposed to be renewed, because we have young turks who are ready to take over.

Concerning retrenchment, when the person has been retrenched is should have all his payment plus the NSSF payments.

Intimidation: The Police officers intimidates on innocent people that the courts cannot prove their guilty or go to research whether the person

Com. Hon Phoebe Asiyo: You have not told what you like and your time is up. Now I just want to explain to give you the list of the people that I have here, that are going to talk next. You have finished, your time is over. We still have these people who are going to give us presentation or just give us their papers. John Sariya Mahero, Penina Asiego, Samson Magomere, Abraham Mwakaguri, and then Juma Engoga is not going to talk he is simply going to hand over the document and then eventually we will have Elizabeth Olado to sing to us. Anybody left out. Mr. John Saiya. Please just give recommendation.

John Sariya Mahero: Mimi naitwa John Sariya Mahero, natoka Ngamarego Sub-Location, Tambua Location, Tiriki West Division.

Pendekezo yangu ni ya kwamba, kwa upande wa utawala ningependekeza ya kwamba Chiefs, ama Assistant Chiefs kimoja kiondelewe. Ningependekeza ma-Assistant Chiefs waondolewe. Halafu tuwe na wazee wa mitaa. Halafu wazee hawa wa mitaa pamoja na chief wachaguliwe direct na wananchi. Ingawa wanaweza kutuma application zao kwa ma-DOs, wafanyiwe mitihani lakini uchaguzi ufanywe na raia wenyewe.

Hukumu ya kinyonga iondolewe. Tuwe na hukumu ya maisha, kama wale wanafungwa maisha. Halafu mtu akifariki kule wenyewe waitwe wapewe maiti.

Kwa ofisi ya Raisi iziwe zaidi na Ministry mbili. Raisi awe chini ya mamlaka.

Wasichana ambao hawakufanikiwa kuolewa, wapewe urithi pamoja na wavulana. Mvulana akipenda msichana ambaye ana watoto ama ana mtoto awachukue wote.

Religious affairs zitoke katika societies.

Kanisa likitaka usajiliwe liwe seconded na zaidi ya Church oriented organization mbili.

Kubuni kwa ministries kukubaliwe na mbunge. Yaani ministries zisitolewe tu na Raisi. Ila zile ambazo zinataka ziongezwe ama sikubaliwe zikubaliwe na Bunge.

Halafu Raisi awe Mbunge ambaye amekuwa kwa Bunge zaidi ya miaka kumi mfululizo. Yangu ni hayo tu mbarikiwe.

Kanisa litoke katika ofisi ya societies. Iwe na idara yao.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asante sana Bwana Sariya. Sasa Mama Penina Asiego, kuna mama alikuja mbele hakujiandikisha hawa mbele ya hawa wengine watatu anaitwa Roselini. Nitaampa dakika moja tu kwa maana alikuja amechelewa na sisi tulikuwa hapa tangu asubuhi. Mama endelea. Sema majina yako, halafu uendelee.

Penina Asiego: *Vananganga Penina Asiego Mahero, nindulanga muluveka lwi Ikamalenga*

Translator: I am called Penina Asiego Mailo from Ngamarenge.

Penina Asiego: *Inzi ni kutanga kusandiza Mwami Yesu mukamba kwa kalunu*

Translator: I will start by praising God.

Penina Asiego: *Uyanzi inzi kwingila mu Church ya African Divine*

Translator: Who has made it possible for me to come to this Israel Nineveh Church.

Penina Asiego: *Nyanzi sana kuli nyoye avakana na vayayi na basakulu nivekaye mchelitsa vosi, milembe vosi.*

Com. Adagala : *Uhula hee umolome mang'ana ka maisha. Ibindu viveye mumaiisha, violola bidinyu sio mkele sio mbugani niko komoloma. Kuli abandi bakamoloma yaha. Isukulu, umolome kenako.*

Penina Asiego : *Inzi simbeye ligali ni cha nyala kuvola ligali ta, ni tali moloma kuluveka lwa kunyi abakele.*

Translator: I don't have much to say but I am going to talk about us women.

Penina Asiego: *Abakele kuve nuvunyanu sana*

Translator: We women are really suffering.

Penina Asiego: *Avala tsingulu tsiaveye kufwa shimunyalitsa kugenda da*

Translator: Some of us have no energy, we cannot even walk.

Penina Asiego: *Makaloleka kuveye no bukonyi kuli unyala kwikonya dawwe*

Translator: It happens that we don't even have any help.

Penina Asiego: *Makaloleka abasakulu batulaho batsia wa Nyasae*

Translator: And our men have died they are not there.

Penina Asiego: *Ku kunyala kwikonya ndi avangunzakali*

Translator: How can we widows be helped.

Penina Asiego: *Munyala kukuhenzelaku kuli kunyala kwikonya sigira kuveye abakele batsililu*

Translator: Can you find away of helping us.

Com. Hon Phoebe Asiyo: How can we help the women. Can't she tell us how.

Penina Asiego: *Nako butswa ndio.*

Translator : *That is all.*

Penina Asiego : *Bakukonye kuli mbunyakani bwitu, sikuveye ligali ni lilia lilahi da, libika lilahi da, mavulwaye vwatsilaho, mbukungu bwene bula ma kulola itsisenti tsiukutsia musipitali sikuveye natsio dave, ku serikali inyala kukukonyaku?*

Translator: We are just asking that you help us in our problems because we don't have any money and if the Government can help us we can be okay.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Okay asante sana Mama. Umefanya vizuri kufika na kuongea vizuri. Tumeshukuru. Sasa huyu Roseline dakika moja tu kwa maana umekuja umechelewa. Na hata jina lako hujaweka kwa register.

Roseline Akinyi Odera: Kwa jina mimi naitwa Roseline Akinyi Odera. Ningependeza kwa sisi wajane tuna-achwa kama wangali wadogo. Tungependa ile pesa tunapewa baada ya miaka tano mume akifa, zingeendelea kutokana ili zitusaidie kwa ajili tunaachwa na watoto wadogo na hizo pesa zinakwisha kama mtoto akiwa kwa darasa la kwanza mpaka darasa la nanae.

Sisi wajane afadhali wangetupatia kazi pale bwana alikuwa akifanya kazi tungeendelea na kazi halafu tungechukua loan kwa ofisi ya Serikali, hiyo ingetusaidia kulipa karo ya secondary schools.

Kazi tutaweza kupewa hata ya kufagia halafu utakuwa utaendelea kufundisha watoto ukichukuwa loan kwa Serikali.

Hizi pesa tunapewa baada ya Bwana akikufa miaka tano inakwisha na labda Bwana alikufa kama angali kijana inapatikana pesa hazitoshi. Sasa kama mimi mjane niliwachwa na watoto wadogo ningependekeza Serikali ingetusaidia watoto wetu wangesoma mpaka darasa la nane bila kulipa karo. Halafu secondary afadhali tungepata watu wengine watusaidie kwa ajili wakati tumewachwa kama tuko wajane, ndugu au dada za marehemu hawawezi kutusaidia. Tumeomba wajane wasaidiwe. Ni hayo tu asanteni.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asante sana Roseline. Sasa tuko Bwana Samson Magomere alikuja alikuja amechelewa, na

tunampa muda mfupi kuongea. Nyuma ya Samson ni Bwana Mwakaguri halafu Juma Amuhaya ambaye ni mwenyekiti wa Supreme Muslim

Council kwa area hii. Wewe ni nani? Nilikuwa mara nyingi sana Philip. Samson Magomere ako wapi ametoroka oh no. Abraham Mwakaguri utafuatwa na Juma Engoga.

Abraham Mwakaguri: Na tumaini ya kwamba majina yangu ni Abraham Mwakaguri. Langu la kwanza ni kuhusu vile watu wamekuwa wakiongea hapa kuhusu mambo ya Majimbo. Kwa hivyo ingawa nilikuwa nimeandika hivyo kitambo naonelea mambo ya majimbo, yasiweko, kwa sababu tukisema majimbo hapa, majimbo pale hatuna Serikali ambayo tutaipeleka ama tutaita. Kwa sababu sisi wote ni raia wa Kenya. Na wazaliwa wa-Kenya na ningependelea mahali mtu alipo akaye pale pale, maana hapo ndipo ili Mungu alipotuweka katika ulimwengu huu.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Lakini kumbuka kwamba majimbo si kusema mtu anahama kutoka mahali anaenda mahali pengine. Endelea.

Abraham Mwakaguri: Jambo la pili ni kuhusu wale ma-MPs wetu katika constituencies, ambao wanataka kura. Ningeonelea ya kwamba, si vizuri katika sehemu moja wasimame watu watano sita, kugombea sehemu hiyo moja. Uzuri tu ni hao kukaa mahali pamoja, katika upendo na wasikizane ni nani ataenda. Baadala ya kutenganisha watu na mwishowe kuwacha watu wakipigana wakimwaga damu.....

Com. Hon Phoebe Asiyo: Siasa hakuna ya mapenzi. Na kung'ang'ania mpaka mtu apate. Lakini umesema endelea na lingine.

Abraham Mwakaguri: Jambo la tatu, ningependa katika Serikali ijao mambo kuhusu ufisadi ukomeshwe kabisa. Kwa sababu sisi raia wengine wa chini tuko na shinda sana kubwa sana. kwa hivyo tunaona saa ingine wakati mtu anapelekwa hapa kotini unakuta kwamba, aneneleka shilingi elfu tano halafu mtu anatolewa tu hapo, wale wengine mbele hawajui.

Mwisho kabisa ningependa Serikali ambayo inakuja iendelee na kuamuru ama tuwe na uhuru wa kuwabudu tusiwe na ule uhuru wa kuwabudu mapepo. Bali tuabudu yule Mungu wetu aliyetumba tuumba tukikaa chini ya upendo, amani, na umoja. Kwa hivyo ni asante.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Asante sana Mzee umefanya vizuri tumeshukuri. Sasa yule wa mwisho halafu tupate nini kwa Elizabeth Olando, atakuwa Bwana Juma, Supreme Council. Nathan ulikuja umechelewa unaingia saa hii. You should be here in the morning because you are very important person. Don't let down your people.

Juma Amuhaya: My names Juma Amuhaya Engonga, nikiwa Chairman wa Supreme Muslim Council of Kenya, Muslimi's in

Vihiga District. Yangu nitaenda haraka haraka nitamwomba mwenye kengele tafadhali.

Yangu ya kwanza ningependa kusema hivi kwa upande wa dini yetu ya Kiislam, vija wa Kislamu wale ambao wamesoma, na wamehitimu vizuri, wamemaliza masomo yao, ningelipendekeza hivi hawa wawe wakiandikwa katika shule za Serikali. Wakati kuna watoto wakiislam wanasoma katika hizo shule, wawe wakiwa hapo ili kuweza kufundisha ma-subjects zingine especially the Holy Koran, na mambo mengine. Fitakuwa ni bora vijana wa-Kiislam walio na masomo kuandikiwa kwenye ma-ofisi ya Serikali, kumbolesha mawasiliano mwema ambao wakati vipande vinaandikishwa wawe wakihakikisha ya kwamba yule mtu ambaye anandikwa kwa kupewa kipande si mu-Somali. Pendekezo langu ni kwamba wahakikishe ya kwamba huyu mtu si Msomali ambaye anaandikishwa, bali ni mwana Kenya.

Vchinjaji wa nyama katika Kenya hii, tumepata shinda nyingi kwa watu wanachinja ngombe huko kwa bush halafu wanailete kwa Butchery wanakuja kuuza hata Mkristo halali, Muislam halali. Pendekezo langu ni kwamba, lazima kuwe na wachinjaji walioteuliwa vizuri, na mihuri ama muhuri iwe ni ya Chairman wa Supreme Muslim Council Vihiga District, ambaye ni mimi mwenywe.

Kitu kingine ambacho ninglipenda kumalizia nacho, naomba ama napendekeza kuwe na koti ya Kislam ambayo ina-deal na wale wanaume Wakislam wenye kunyanyasa akina mama. That is wanaweza kukuta yaani wakati ametoka tu mahali ametoka ana fikiria lazima ni mfukuze mke wangu vile ni desturi ya Kiislam lazima talaka itolewe ana peana talaka bila kufikiria. Kwa hivyo sisi tunaomba Serikali yetu ya Kenya, wakati inatupatia Kadhi, wakati mtu anapofanya ndoa, wapime akili zake na kuona huyo mtu mwenye kufanya arusi akili yake ni timamu kabisa. Asiweze kumyanyasa mke wake wa ndoa.

Nafikiri kumalizia kabisa yangu ya mwisho, mimi ningelipendelea hivi, kwa upande wa Serikali, wa kuteuwa Councillors, kuna mtu ambaye ameteuliwa na vote, mwingine amekuwa nominated. Naomba Serikali ama pendekezo langu ni kwamba Serikali, huyu wa-kwanza akipita, number two awe taken in, wasiwe waki-pack tu kwa sababu mtu ni rafiki ya fulani wanakwenda kwokota mtu wanasema we have nominated so and so when he doesn't or she doesn't qualify. Nafikiri kwa hayo machache wakati umekuwa ni mfupi dear Commissioners, Mungu atawabariki mahali mtaenda.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Tumeshukuru sana ulifika umechelewa ungesema zaidi. Sasa Elizabeth Olado.

Elizabeth Olando: Kwa majina ni Elizabeth Olado.

Fanya kazi ya Katiba pole pole, fanya kazi ya Katiba pole pole, Usije ukasema, usije ukasema, Katiba yangu imenifinya.

Panga mambo ya Katiba pole pole, Panga mambo ya Katiba pole pole

Usije ukasema, usije ukasema, Katiba yangu imenifinya.

Panga kazi ya vilema pole pole

Panga kazi ya vilema pole pole

Usije ukasema, usije ukasema, Katiba yangu imenifinya.

Panga mambo ya vijana pole pole

Panga mambo ya vijana pole pole

Usije ukasema, usije ukasema, Katiba yangu imenifinya.

Panga mambo ya wajane pole pole

Panga mambo ya wajane pole pole

Usije ukasema, usije ukasema, Katiba yangu imenifinya.

Com. Hon Phoebe Asiyo: Thank you. Sikutaka huo wimbo uimbiwe kabla hatujamaliza ndio nimemuuliza Elizabeth akae mpaka muda huu wa mwisho. Sasa nina furaha kwamba ninyi nyote mumekuja na mumekaa na sisi mpaka wakati huu wa mwisho. Natoa asante sana kwa maoni yenu na kwa wale ambao pia walikuja kuzikiliza. Tunajua kwamba wakati ukifika wa kuleta repoti hapa ya constituency wale walihuduria hapa tena watahudhuria yale waongewe juu ya hiyo riporti muone kweli ile mambo mliotweleza tuliandika vile mliyokuwa mumetaka. Halafu baadaye vile nilieleza pale mbeleni, pengine kulikuwa na wengine ambao hawajafika. Mwishoni tutakuwa na National Conference, ambayo itaangalia mapendekezo yote ambayo mliuambia kwa Kenya nzima wakipitisha basi mambo haya enda kwa Bunge na tutapata Katiba mpya. Na itakuwa ni kazi na jambo nzuri sana kwa wa-Kenya kupokea Katiba mpya kwa maana kwa miaka kumi sasa au zaidi ya miaka kumi, wana-Kenya wamejaribu sana wapate Katiba mpya. Huu ni wakati unaofaa waweze kupata Katiba hiyo na tunaomba Mwenyezi Mungu kwamba itakuwa vile watu wa Kenya walitaka iwe na ipendeze pia Mungu Mwenyezi. Sasa tunafunga na vile tulivyoanza tungeuliza mzee mmoja wa kanisa atuombea au yeyote anayeweza kutuombea , mzee sasa maana tulikuja kanisa lako ulikuwa hauko. Sasa utatuombea tukifunga. Hapa fika hapa mbele ushike hiyo micro-phone utuombea halafu utasema jina lako maana hiyo maombi yako itaingizwa kwa kitabu chetu na mpaka tujue alitoa maombi hayo.

John Mweleza Kiburi :Tunaweza kuheshimu. Tusimame zote. Tunataka kuomba tafadhalini. Kwanza on behalf of the members of African Nineveh Church and also those coming from Hamisi constituency, I would like to wish you the best as you travel from this place and it has been very good to receive you all in this place of ours. So where ever you go, we want to wish you God's blessings and in whatever you are doing, may God help you in everything you do.

And on behalf of the members of African Nineveh Church International also could we may wish to welcome you, we shall be having sixty years celebration since this church was founded in 1942, and if you get any opportunity you are welcomed to the celebration that will take ten days. All of you are most welcome.

My name is John Mweleza Kiburi the 2nd, I am the Arch-bishop of this church but currently I am in the UK I am doing my Phd. so I am just over here doing my research.

May we pray: Asante Baba wetu tuna kushukuru kwa sababu unatupenda na kwa sababu tuko hapa, tunajua ya kwamba ni mpango wako ulikuwa umepanga tangu zamani hata kabla ya kuumbwa ulimwengu na hata si wenyewe kuzaliwa. Baba tunataka kukabidhi watumishi wako mkononi mwako, wale ambao wamefika hapa wakiongozwa na Professor Ghai, Mwenyezi Mungu utakuwa pamoja nao, uwabariki na wengine wote ma-Commissioners walio hapa uzidi kuwalinda. Baba naweka watu wako wote ambao wanaishi katika sehemu hii ya Tiriki, ukazidi kuwabarikia mipango yao yote na yote ambayo wamezungumza hapa, Baba ukazidi kuwa Mungu wao. Baba kila mmoja ambaye yuko hapa anapojiandaa kuondoka hapa, na kwenda nyumbani tunataka kuamini ya kwamba utakuwa kiongozi wa kila mmoja, na mabaya katika safari na ajali utaweza kuwasidia tunajuwa ya kwamba una uwezo na unaweza kutenda haya kwa sababu umesema mahali wamekaa wawili watatu, chochote watasikizana wewe pia utakubali kule Mbinguni. Watu wako wametoa maoni ya aina mbali mbali Mwenyezi Mungu uzidi kuwasaidia ma-Commissioners, wanapokwenda kuyaangalia haya matatizo yetu na kuyaweka katika mipango ambayo inafaa utawasaidia na kuwapa akili zuri na utawapa uzima mzuri, ili waweze kutenda haya yote. Nataka kuwamini ya kwamba watu wako hapa, wanapoondoka hapa ukazidi kuwabariki popote wanapotembea, katika jina safi la Yesu Christo Mukombozi wetu Amen. mbarikiwe nyote.

XXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXX